# WARAKA WA TATU WA YOHANA

1 Mimi mzee nakuandikia wewe Gayo, rafiki
yangu, ninayekupenda kweli. 2 Mpenzi wangu,
nakutakia mafanikio mema ya kila aina;
nakutakia afya njema ya mwili kama ulivyo
nayo rohoni. 3 Nimefurahi sana ndugu kadhaa
walipofika hapa, wakaiambia juu ya uaminifu
wako kuhusu ukweli; naam, wewe unaishi daima
katika ukweli. 4 Hakuna kitu kinachonifurahisha
zaidi kuliko kusikia kwamba watoto wangu
wanaishi katika ukweli. 5 Mpenzi wangu, wewe ni
mwaminifu kila mara unapowahudumia ndugu,
hata kama ni wageni. 6 Ndugu hao wamelieleza
kanisa hapa habari za upendo wako. Tafadhali
uwasaidie waendelee na safari yao kwa namna
itakayompendeza Mungu, 7 Maana wanaanza
safari yao katika utumishi wa Kristo bila kupokea
msaada wowote kutoka kwa watu wasioamini.
8 Basi, sisi tunapaswa kuwasaidia watu hawa,
ili nasi tupate kushiriki katika kazi yao kwa
ajili ya ukweli. 9 Niliandika barua fupi kwa
hilo kanisa; lakini Diotrefe, ambaye hupenda
kuwa kiongozi wao, hataki kabisa kunisikiliza.
10 Basi, nitakapokuja nitayafichua mambo yote
anayofanya, maneno mabaya anayotutolea
na uongo anaosema juu yetu. Isitoshe, yeye
hukataa kuwakaribisha hao ndugu walio safarini,
na hata huwazuia watu wengine wanaotaka
kuwakaribisha, na hujaribu kuwafukuzia nje

ya kanisa. 11 Mpenzi wangu, usifuate mfano
mbaya, bali mfano mwema. Kila atendaye
mema ni wa Mungu; lakini anayetenda mabaya
hajapata kumwona Mungu. 12 Kila mtu anamsifu
Demetrio; naam, ukweli wenyewe unamsifu.
Nasi pia tunatoa ushahidi wetu juu yake, nawe
wajua kwamba tunachosema ni kweli. 13 Ninayo
bado mengi ya kukwambia, lakini sipendi
kuyaandika kwa kalamu na wino. 14 Natumaini
kukuona karibuni na hapo tutazungumza ana
kwa ana. (G1-15) Nakutakia amani. Rafiki zako
wanakusalimu. Wasalimu rafiki zetu wote kila
mmoja binafsi.

# Biblia Takatifu
## Portions of the New Testament in the Swahili Language of Kenya, Mozambique, Somalia, and Tanzania, translation by Dr. Johann Ludvig Krapf completed in 1850

Public Domain

Language: Kiswahili (Swahili)

Dialect: Kimvita

Translation by: Dr. Johann Ludvig Krapf

2014-08-25

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 11 Nov 2022 from source files dated 9 Oct 2020
62071dc0-70e6-5b86-b569-c1b45e7771bd